# Ofisi ya Taifa ya Takwimu

S. L. P 796 Simu: 255- (022) 2122722/3/4 Nukushi:+225 (022)

Dar es Salaam,-TANZANIA Barua pepe: dg@nbs.go.tz


***Unapojibu tafadhali taja:*** **YALIYOJITOKEZA**

**Kumb Na: NBS/S.40/21/461** **Tarehe: 15 Februari, 2012**

## FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA MWEZI JANUARI, 2012

## Utangulizi

### Maana ya Fahirisi za Bei za Taifa

Fahirisi za bei za Taifa ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazotumiwa na jamii. Bei za bidhaa na huduma zipatazo 224 hukusanywa kila mwezi kwa kila mkoa nchini.

### Mizania mpya za bidhaa na huduma za jamii na kizio cha bei

Mizania ya Fahirisi za bei za Taifa zimetokana na matumizi ya kaya binafsi kutoka mikoa 21 ya Tanzania Bara. Mizania inajumuisha matumizi ya kaya zote binafsi kutoka mijini na vijijini. Kizio cha Fahirisi za Bei za Taifa kimebadilishwa kutoka Desemba 2001=100 hadi Septemba 2010=100.

### Makundi ya bidhaa na huduma za jamii

Marejeo ya Fahirisi za Bei za Taifa yamefanyika kwa kufuata makundi yaliyokubalika Kimataifa yanayoitwa mchanganuo wa matumizi binafsi "Classification of Individual Consumption by Purpose (COICOP)". Fahirisi mpya za Bei inajumuisha makundi 12 ya mfumo wa COICOP pamoja na fahirisi za bei kwa makundi maalumu. Makundi hayo maalumu ni; 1) Vyakula na vinywaji baridi—vikijumuisha vyakula vinavyoliwa majumbani na mahotelini; 2) Nishati na Mafuta - kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli; 3) Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi; 4) Fahirisi za huduma zote za jamii isipokuwa vyakula, vinywaji baridi, nishati na mafuta.

### Namna ya kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa

Maboresho yamefanyika kwenye ukokotoaji wa Fahirisi mpya za Bei za Taifa, ikiwa ni pamoja na kutumia wastani wa jiometria "geometric means" kwenye kukokotoa Fahirisi za Bei katika ngazi za mwanzo badala ya wastani wa kawaida "arithmetic mean", matumizi ya mfumo ulioboreshwa wa ukokotoaji pamoja na mfumo mzima wa kukusanya na kuchambua bei. Kanuni ya "modified Laspeyres index" inaendelea kutumika kukokotoa Fahirisi za Bei za Taifa katika ngazi ya makundi makubwa.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWAKA UMEPUNGUA KIDOGO HADI ASILIMIA 19.7

### Jedwali Namba 1: Badiliko la Fahirisi za Bei za Taifa kwa Mwezi Januari 2012 (Septemba 2010 = 100)

| Na. | KUNDI (MAIN GROUP) | Mizania (Weight) | Jan-2011 | Des - 2011 | Jan - 2012 | Badiliko la mwezi mmoja | Badiliko la miezi 12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vyakula na vinywaji baridi | 47.8 | 106.16 | 131.09 | 135.72 | 3.5 | 27.8 |
| 2 | Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku | 3.3 | 100.95 | 106.59 | 107.35 | 0.7 | 6.3 |
| 3 | Mavazi ya nguo na viatu | 6.7 | 102.54 | 112.96 | 115.40 | 2.2 | 12.5 |
| 4 | Nishati, Maji na Makazi | 9.2 | 103.84 | 122.64 | 123.34 | 0.6 | 18.8 |
| 5 | Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba | 6.7 | 102.84 | 116.10 | 117.64 | 1.3 | 14.4 |
| 6 | Gharama za Afya | 0.9 | 100.41 | 103.38 | 103.83 | 0.4 | 3.4 |
| 7 | Usafirishaji | 9.5 | 101.32 | 112.34 | 112.34 | 0.0 | 10.9 |
| 8 | Mawasiliano | 2.1 | 98.48 | 98.14 | 98.06 | -0.1 | -0.4 |
| 9 | Utamaduni na Burudani | 1.3 | 98.74 | 101.13 | 103.16 | 2.0 | 4.5 |
| 10 | Elimu | 1.7 | 104.88 | 105.79 | 107.89 | 2.0 | 2.9 |
| 11 | Hoteli na Migahawa | 6.4 | 103.56 | 113.99 | 116.86 | 2.5 | 12.8 |
| 12 | Bidhaa na huduma nyinginezo | 4.5 | 99.97 | 108.60 | 109.06 | 0.4 | 9.1 |
| | **JUMLA – FAHIRISI BIDHAA ZOTE** | **100.0** | **104.10** | **121.79** | **124.64** | **2.3** | **19.7** |
| | **Makundi Mengine Teule** | | | | | | |
| 1 | Vyakula na vinywaji baridi—vikijumuisha vyakula vilivyoliwa majumbani na mahotelini | 51.0 | 105.88 | 129.20 | 133.63 | 3.4 | 26.2 |
| 2 | Nishati na Mafuta—kundi hili linajumuisha umeme na aina nyingine za nishati zinazotumika majumbani pamoja na petroli na dizeli | 5.7 | 101.61 | 134.25 | 132.24 | -1.5 | 30.1 |
| 3 | Fahirisi za bidhaa na huduma zote za jamii isipokuwa vyakula na vinywaji baridi | 49.0 | 102.00 | 113.03 | 114.00 | 0.9 | 11.8 |
| 4 | Fahirisi na huduma zote za jamii Isipokuwa vyakula, nishati na mafuta | 43.3 | 102.06 | 109.84 | 111.26 | 1.3 | 9.0 |

Mfumuko wa Bei wa Taifa wa mwaka unapima kiwango cha badiliko la kasi ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Jedwali namba 1 hapo juu linaonyesha kwamba, mfumuko wa bei wa Taifa kwa mwezi Januari 2012 umepungua hadi asilimia 19.7 kutoka asilimia 19.8 kwa mwezi Desemba 2011. Kupungua kwa Mfumuko wa Bei wa mwezi wa Januari 2012 kunamaanisha kuwa, kasi ya upandaji wa bei za bidhaa na huduma kwa mwezi Januari 2012 imepungua ikilinganishwa na kasi ya kupanda kwa bei kwa mwezi Januari 2011. Hata hivyo, kwa ujumla Fahirisi za bei zimeongezeka hadi 124.64 kwa mwezi wa Januari 2012 kutoka 104.10 kwa mwezi wa Januari 2011. Vyakula na Vinywaji Baridi vimeongezeka kidogo hadi asilimia 27.8 mwezi wa Januari 2012 kutoka asilimia 27.1 kwa mwezi wa Desemba 2011.

### Mfumuko wa Bei kwa Bidhaa za Vyakula na Bidhaa Zisizo za Vyakula


Badiliko la Fahirisi ya Bei za bidhaa za vyakula majumbani na migahawani limeongezeka hadi asilimia 26.2 kwa mwezi wa Januari 2012 ikilinganishwa na asilimia 25.6 kwa mwezi wa Desemba 2011. Kasi ya ongezeko kwa bidhaa zisizo za vyakula imepungua kidogo hadi asilimia 11.8 kwa mwezi wa Januari 2012 kutoka asilimia 12.7 kwa mwezi wa Desemba 2011.

## Mfumuko wa Bei wa Bidhaa na Huduma Zote Isipokuwa Bidhaa za Vyakula na Nishati

Aina hii ya Fahirisi haijumuishi vyakula vilivyoliwa majumbani na migahawani, vinywaji baridi, petroli, dizeli, gesi ya kupikia, mafuta ya taa, mkaa na umeme. Vyakula na nishati vina sifa ya kuwa na bei ambazo hubadilika mara kwa mara hivyo vikiondolewa kwenye Fahirisi ya bidhaa na huduma zote hubakia Fahirisi ambayo ina mwelekeo imara kwa watunga sera.

Mfumuko wa bei ambao haujumuishi vyakula na nishati kwa mwezi wa Januari 2012 umeongezeka hadi asilimia 9.0 kutoka asilimia 8.7 kwa mwezi wa Desemba 2011. Kwa upande mwingine, mfumuko wa bei wa nishati umepungua hadi asilimia 30.1 kwa mwezi wa Januari 2012 kutoka asilimia 41.0 kwa mwezi wa Desemba 2011. Kupungua kwa mfumuko wa bei wa nishati kumesababishwa hasa na kupungua kwa bei za mkaa kwa asilimia 0.7 na mafuta ya taa kwa asilimia 2.3. Badiliko kidogo kwenye bei ya mkaa kuna athari kubwa katika fahirisi za nishati na mafuta kwani mkaa unachukua zaidi ya nusu (asilimia 2.5) ya matumizi yote (asilimia 4.7) ya kundi hilo.

**Kielelezo Namba 1: MWELEKEO WA FAHIRISI ZA BEI ZA TAIFA NA MFUMUKO WA BEI KUTOKA JANUARI, 2011 HADI JANUARI, 2012. (SEPTEMBA 2010 = 100)**




Kielelezo namba 1 hapo juu kinaonesha kuwa, katika kipindi kati ya Januari 2011 hadi Januari 2012, kumekuwa na mwenendo wa kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma mbalimbali kama inavyooneshwa na Fahirisi za bei. Mfumuko wa bei umekuwa na mwenendo wa kupanda kutoka asilimia 6.4 mwezi Januari 2011 hadi kufikia asilimia 19.8 mwezi Desemba 2012 na kupungua kidogo hadi asilimia 19.7 mwezi Januari 2012.

## MFUMUKO WA BEI KWA KIPIMO CHA MWEZI UMEONGEZEKA KWA ASILIMIA 2.3

Mfumuko wa Bei wa mwezi Januari 2012 umeongezeka kwa asilimia 2.3. Fahirisi za Bei zimeongezeka hadi 124.64 mwezi Januari 2012 kutoka 121.79 mwezi Desemba 2011. Kuongezeka kwa mfumuko wa bei kumechangiwa na kuongezeka kwa bei za bidhaa za vyakula na zisizo za vyakula. Baadhi ya bidhaa za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa bei ni pamoja na mchele kwa asilimia 13.6, mikate kwa asilimia 2.4, unga wa ngano kwa asilimia 3.9, nyama kwa asilimia 2.0,

samaki kwa asilimia 5.2, maziwa kwa asilimia 2.7, mayai kwa asilimia 3.4 na mbogamboga kwa asilimia 5.6. Kwa upande mwingine, baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa bei ni pamoja na bia kwa asilimia 0.7, suti za wanaume kwa asilimia 9.7, sare za shule ya msingi kwa asilimia 3.5, kodi ya nyumba kwa asilimia 6.5, magurudumu ya magari kwa asilimia 4.3, madaftari kwa asilimia 4.8, ada ya shule za msingi za binafsi kwa asilimia 5.0, ada ya shule za sekondari za binafsi kwa asilimia 2.9 na sabuni za kufulia kwa asilimia 6.5.


## Thamani ya Shilingi ya Tanzania Mwezi Septemba 2010 Ikilinganishwa na Mwezi Januari 2012

Tafsiri: Thamani ya Shilingi ya Tanzania inapima badiliko la uwezo wa Shilingi ya Tanzania katika kununua bidhaa na huduma mbalimbali za mlaji ambazo Shilingi ya Tanzania itaweza kununua katika vipindi tofauti. Ikiwa wastani wa Bei za Taifa (Fahirisi) unaongezeka, thamani ya fedha hupungua.

Thamani ya shilingi 100 imepungua kutoka mwezi Septemba 2010 hadi kufikia Shilingi 80 na senti 23 mwezi Januari 2012.

## MIENENDO YA BEI

### Kielelezo Namba 2: Mienendo ya Bei kwa Makundi Mbalimbali ya Fahirisi za Bei




Kielelezo namba 2 hapo juu kinaonyesha mienendo ya bei kwa makundi mbalimbali ya fahirisi za bei kuanzia mwezi Januari 2011 hadi mwezi Januari 2012. Kwa wastani, Fahirisi za vyakula na vinywaji baridi na Fahirisi za nishati na mafuta zimekuwa na mwenendo wa juu kwa kipindi chote zikilinganisha na fahirisi zingine isipokuwa mwezi wa Januari 2012 Fahirisi za nishati na mafuta zimeshuka kidogo. Kundi la nishati na mafuta limeonyesha pia kuwa na mwenendo wa fahirisi usio imara ikilinganishwa na makundi mengine kwa kipindi husika. Fahirisi za bidhaa zisizo za chakula na fahirisi za bidhaa zisizo za chakula pamoja na nishati zimeonesha mwenendo wa bei ulio imara.

**Mawasiliano: Mkurugenzi Mkuu,**

**Ofisi ya Taifa ya Takwimu**